


NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko vifaa vya kukamulia na kuhifadhia maziwa kwa niaba ya Chama cha Ushirika Mkoa wa Katavi wakati wa kufunga kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Unywaji Maziwa iliyofanyika mkoani Katavi, jana. (Picha na [illegible])

# Kitita cha fedha kutolewa kwa watakaofich

Scanned with CamScanner




vestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega (R) has a word with NMB Bank Plc officers earlier this week when he visited the bank's pavilion during e closure of the Tanzania Dairy Board exhibitions held in Katavi Region. He praised the bank for expressing readiness to issue soft-term loans to farmers and storalists. Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner



## HABARI ZA BIASHARA

# Wazalishaji maziwa wapewa mbinu ya masoko

Na Mwandishi Wetu, Katavi

WAZALISHAJI wa maziwa na bidhaa zake wameshauriwa kuthibitisha ubora wake, hatua itakayosaidia kuwaongezea masoko na tija kwenye bidhaa hizo.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Uhusiano wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Neema Mtemvu kwenye maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika kwenye viwanja vya Azimio mkoani Katavi.

Neema alisema TBS imeshiriki maonesho hayo kwa lengo la kuwasogezea huduma karibu wazalishaji wa maziwa kwa kuwapatia elimu ya viwango ili waweze kuzalisha bidhaa bora na salama zinazoweza kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi. Alisema nchi za Afrika Mashariki zina makubaliano kuhusiana na bidhaa zilizothibitishwa ubora na kila mzalishaji aliyethibitisha ubora wa bidhaa yake ni ruksa kupeleka bidhaa hizo katika nchi yoyote katika ukanda bila kukumbana na vikwazo vya kibiashara.

"Huduma ya uthibitishaji ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali wadogo ni bure, kinachotakiwa ni wajasiriamali kupata barua ya utambulisho kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kuipeleka TBS, ambapo mchakato wa kuwapatia alama ya ubora unaanza mara moja," alisisitiza.

Alisema TBS inatambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza pato la taifa na kutengeneza ajira kwa wananchi wengi, ndiyo maana kuna mchakato endelevu wa kutoa elimu kwa wajasiriamali kwa kuwa na hilo ni sehemu ya majukumu ya shirika ili waweze kupata alama ya ubora.

Aidha, alisema kupitia maonesho hayo walitoa elimu kwa wananchi kuhusiana na masuala ya viwango na kuwataka waelewe kwamba vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee, bali ni jukumu la kila mwananchi.

Alisema wananchi hao walielimishwa umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku pamoja na kuwafahamisha fursa ya huduma ya kuthibitisha bure bidhaa inayotolewa kwa wajasiriamali wadogo.

Kwa mujibu wa Neema, mbali ya kutoa elimu kwa wananchi hao kuhusu masuala ya viwango wametakiwa kuhakikisha wanakuwa mabalozi kwa kuhamasisha kutumia bidhaa bora katika jamii wanazoishi.

Aliwataka wananchi waliofika kuhudhuria maonesho hayo kutoa taarifa kwa shirika wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko.

Scanned with CamScanner



# TBS counsels milk producers, processors in Katavi